



Australian Government

COVID-19
✓ **VACCINATION**

Nani watapata chanjo ya COVID-19, na wapi?



Kila mtu nchini Australia anaweza kupata chanjo bure ya COVID-19, hata ikiwa hana kadi ya Medicare.

Lakini sio kila mtu anayeweza kupata chanjo kwa wakati huo huo.



Kila mtu nchini Australia anahimizwa kupata chanjo ili kusaidia kujikinga yeye mwenyewe na jamii dhidi ya ugonjwa wa COVID-19.



Makundi mengine ya watu yanaweza kupata chanjo ya COVID-19 kabla ya wengine. Makundi hayo yanajumuisha watu ambao wako katika hatari zaidi ya:

- kuambukizwa na virusi
- kuwa wagonjwa sana wakiambukiza na virusi.

Hawa wanaitwa **makundi ya kipaumbele**. Kwa maelezo juu ya nani anayeweza kupata chanjo ya COVID-19, angalia: www.health.gov.au/initiatives-and-programs/covid-19-vaccines/getting-vaccinated-for-covid-19/when-will-i-get-a-covid-19-vaccine

Watu wa kwanza kuchanjwa wanajumuisha:



- madaktari na wafanyakazi wengine wa afya
- watu wenye umri wa juu ya miaka 70
- watu wanaoishi katika makazi ya wazee
- watu wanaofanya kazi katika makazi ya wazee
- wafanyakazi wa karantini na wa mipakani
- watu wanaofanya kazi katika huduma ya ulemavu
- watu wanaofanya kazi fulani, kama polisi na wazima moto

- watu wenye ulemavu
- watu wenye matatizo makubwa ya afya
- watu wa Asili na wa visiwa vya Torres Strait wenye umri wa miaka 50 na zaidi.



Kuanzia tarehe 8 Juni, watu wanaotajwa hapa chini wanastahiki:

- watu wazima wenye umri miaka 40 na kupanda juu
- watu wa Asili na wa visiwa vya Torres Strait wenye umri wa miaka 16-49
- watunzaji wa watu wenye ulemavu
- baadhi ya wamiliki wa viza vya muda ambao wanahitaji kusafiri



Watu wanaobaki watastahiki baadaye:

- Watu wenye umri wa miaka 16-39.
- Watu wenye umri chini wa miaka 16.


Unaweza kupata chanjo ya COVID-19 wapi?



Unaweza kupata chanjo kutoka maeneo mbalimbali.

Maeneo hayo yanajumuisha:

- kliniki ya daktari wa familia ya mtaani
- kliniki za afya au za matibabu katika eneo lako
- kliniki za chanjo za serikali.



Hakuna haja kuwa na kadi ya Medicare ikiwa unatembelea kliniki ya chanjo ya serikali.

Jinsi gani kuweka nafasi kwa chanjo yako



Unaweza kujua wapi unapoweza kuweka uteuzi kwa kuwasiliana na mahali panapotoa chanjo.



Unaweza kuona orodha ya maeneo yanayotoa chanjo kwa kutumia Ukaguzi wa Ustahiki wa Chanjo ya COVID-19 kwa:

covid-vaccine.healthdirect.gov.au/eligibility



Unaweza pia kutafuta kujua unapoweza kupata uteuzi kwa kuongea na daktari wako.



Kutakuwa na chanjo za kutosha za COVID-19 kwa kila mtu nchini Australia, lakini huenda kungoja hadi unapoweza kupata uteuzi kwa chanjo yako kwa sababu maeneo mengine yanaweza kukosa nafasi kwa muda.

Maelezo zaidi



Unaweza kutembelea tovuti ya Idara ya Afya kwa www.health.gov.au/covid19-vaccines-languages ili kupata habari zaidi juu ya chanjo katika lugha yako.



Unaweza kupiga simu kwa Laini ya Msaada wa Virusi vya Korona ya Kitaifa kwenye **1800 020 080**.

Ikiwa unahitaji habari katika lugha nyingine mbali ya Kiingereza, pigia simu Huduma ya Utafsiri na Ukalimani kwenye **131 450**.